# Jamii ya kusini yahamasika katika uhifadhi wa misitu

***Na J.M Frank, Kilwa Masoko***

Hakika yaliyopita si ndwele tugange yajayo,nianze kwa kauli hii kwa kuwa wanaofahamu vizuri kanda ya kusini wasingekubali mabadiliko chanya ambayo wananchi wa kusini wanayo leo hii.

Misitu ni raslimali muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku hivyo ni jukumu letu kama jamii kushiriki kwa dhati katika utunzaji,ili tuweze kunufaika na raslimali zitokanazo na misitu mfano maji, hewa safi na raslimali zitokanazo na misitu ambazo moja kwa moja huchangia maendeleo katika jamii zetu na taifa kwa ujumla.

Kwa wanao ifahamu vizuri kanda ya kusini inakuwa vigumu kukubali mabadiliko yangewezekana katika jamii ya kusini na kuwa wao ni washiriki wakubwa katika kutunza misitu yao.

Mtandao wa jamii wa usimamizi wa misitu tanzania MJUMITA kupitia mradi wa HAKI **KATIKA MISITU** wamefanya na wanaendelea kufanya jitihada kubwa ya kuziunganisha jamii

zinazoishi pembezoni mwa misitu katika kanda ya kusini kuwa na sauti na nguvu ya pamoja katika kusimamia misitu yetu katika kanda hii kwa manufaa ya wanajamii na vizazi vijavyo.

Katika kipindi kifupi cha uraghabishi mitandao hii katika jamii imeonekana kuhamasika kwa kiasi kikubwa kwa kuonyesha nia ya dhati ya kusimamia raslimali zao kwa manufaa ya wanajamii,mitandao mingi imeanzishwa na mingine ipo kwenye hatua mbalimbali za uanzishwaji,mitandao ambayo tayari imenzishwa imeonyesha ushiriki mkubwa katika kuhakikisha wanasimamia rasilimali za misitu kwa manufaa ya jamii na taifa kwa ujumla.
Kwa wanofahamu hali ya utawala wa misitu nchini hasa katika ngazi ya vijiji, haikuwa jambo rahisi kwa

Shehena ya mkaa na mbao zilizokamatwa ya halmashauri ya wilaya ya Kilwa hivi karibuni. Kufanikiwa kukamatwa kwa mbao na mkaa huo kulifuatia taarifa zilizotolewa na baadhi ya wananchi wakiwemo WANAMJUMITA kwa afisa misitu wa wilaya

mwananchi wa kawaida kuchukua simu yake na kumpigia afisa misitu wa wilaya na kutoa taarifa za uvunaji haramu katika eneo lake au kuhoji uhalali wa mvunaji mwenye kibali kuvuna katika eneo lisiloruhusuwa kisheria kuvunwa. Hali hii ndio tunayoishuhudia katika kanda ya kusini, wananchi wamehamasika mno na ni moja ya matokeo ya haraka ya shughuli mbali mbali za mradi huu ambao umekuwa ukitoa mafunzo mbali mbali kwa wanamtandao na wananchi kwa ujumla ili wameze kutambua haki zao katika rasilimali misitu na kuwa tayari kuzidai pale zinapopindishwa.

Sasa ni wajibu wadau mbalimbali wa misitu ikiwepo viongozi wa wakala wa misitu Tanzania, idara za misitu wilaya, serekali za wilaya na vijiji kwa sauti na ushirikiano wa pamoja kuwaunga mkono wanajamii kama chanzo muhimu cha taarifa na washirika wakubwa katika utunzaji na usimamizi wa misitu nchini.
Baadhi ya matukio ambayo ushiriki wa jamii umekuwa wa wazi ni pamoja na:-

1. Kutoa taarifa kwa afisa misitu wa wilaya ya Kilwa, taarifa ambayo ilifanikisha kukamatwa kwa mbao ngapi? zilizokuwa zimevunwa kinyume cha sheria katika mkoa wa Lindi, mbao hizi zilikuwa tayari kwenye jahazi kusafirishwa kwenda Zanzibar.

2. Wananchi wa wilaya ya Tunduru kama wanamtandao wamewewezesha kukamatwa kwa mbao na meno ya tembo yaliyokuwa yakisafirishwa kinyume na sheria.

Mifano hii michache katika kipindi kifupi cha mradi tutakubaliana kwa pamoja kuwa wanajamii ni wadau muhimu kabisa katika kusimamia rasilimali za misitu na hivyo ni muhimu kuendelea kuwatia moyo kwa kuhakikisha tunashuhulikia taarifa zao pindi zinapofikia mamlaka mbali mbali ya nchi yaliyowekwa kwa ajili ya kulinda rasilimali za nchi hii.

Nimalizie kwa kusema kanda ya kusini (Lindi na Mtwara) tunaweza kusimamia rasilimali zetu za misitu tukiwa na dhamira ya dhati na ushiriki wa pamoja. Je, kanda nyingine vipi?